

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**



**MUHTASARI WA SOMO LA HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI
ELIMU YA SEKONDARI KIDATO V-VI
2023**

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2023

Toleo la Kwanza, 2023

ISBN: 978-9987-09-740-1

Taasisi ya Elimu Tanzania

Eneo la Mikocheni

132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi

S.L.P 35094

14112 Dar es Salaam.

Simu: +255 735 041 168 / 735 041 170

Baruapepe: director.general@tie.go.tz

Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (2023). Muhtasari wa Somo la *Historia ya Tanzania na Maadili Elimu ya Sekondari Kidato cha V – VI*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kudurufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

Yaliyomo

Orodha ya Majedwali.....	iv
Vifupisho	v
Shukurani	vi
1.0 Utangulizi.....	1
2.0 Malengo Makuu ya Elimu	1
3.0 Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI	2
4.0 Umahiri wa jumla Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI	3
5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi.....	3
6.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi katika Mchakato wa Ufundishaji na Ujifunzaji	5
6.1 Mwalimu.....	5
6.2 Mwanafunzi.....	6
6.3 Mzazi	7
7.0 Mbinu Pendekewza za Ufundishaji na Ujifunzaji.....	7
8.0 Upimaji wa Maendeleo ya Ujifunzaji.....	8
10 .0 Idadi ya Vipindi	9
11 .0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji	9
Kidato cha V	10
Kidato cha VI	36
Bibliografia.....	59


Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi V-VI.....	4
Jedwali Na. 2: Mgawanyo wa Alama za Upimaji.....	8
Jedwali Na. 3: Maudhui ya Kidato cha V.....	10
Jedwali Na. 4: Maudhui ya Kidato cha VI.....	36

Vifupisho

TET Taasisi ya Elimu Tanzania

TEHAMA Teknolojia ya Habari na Mawasiliano



Shukurani

Maandalizi ya muhtasari wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili Elimu ya Sekondari Kidato cha V–VI yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za Serikali na binafsi. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatoa shukurani za dhati kwa wataalamu wote waliohusika wakiwemo wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule, walimu, wakuza mitaala pamoja na wataalamu kutoka asasi zisizo za kiserikali. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Kusimamia Kazi ya Maboresho ya Mitaala ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yameandaliwa kwa kuzingatia lengo kuu la mabadiliko ya Mtaala wa Mwaka 2023 ambalo ni kuwa na wahitimu wenye ujuzi, maarifa na stadi zitakazowawezesha kuajirini, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku. Pia, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.



Dkt. Aneth A. Komba

Mkurugenzi Mkuu

Taasisi ya Elimu Tanzania

1.0 Utangulizi

Somo la Historia ya Tanzania na Maadili ni somo la lazima kwa mwanafunzi anayejiunga Kidato cha V-VI. Lengo la kujifunza somo hili ni kumjengea mwanafunzi maarifa, ujuzi na mwelekeo utakaomwezesha kukabiliana na mazingira yanayomzunguka katika maisha ya kila siku. Aidha ujifunzaji wa somo hili utamwezesha mwanafunzi kulinda historia ya Tanzania, urithi na maadili ya taifa lake. Vilevile mwanafunzi atawezekuishi kulingana na maadili ya Kitanzania kama vile uadilifu, utu, heshima kwa wote na uzalendo. Aidha, ujifunzaji wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili utamwezesha mwanafunzi kujenga hoja shawishi zinazotokana na utafiti aliofanya kwenye somo hili na litatoa fursa ya kujajiri au kuajiriwa.

Aidha, muhtasari huu umeandaliwa ili kuongoza ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili Kidato cha V-VI katika Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Muhtasari huu unatafsiri umahiri uliobainishwa kwenye Mtaala wa Elimu ya Sekondari hatua ya Juu wa mwaka 2023. Muhtasari unatoa maelekezo ya kumwezesha mwalimu kuandaa mchakato wa ufundishaji kwa ufanisi. Pia, muhtasari huu unatoa nafasi kwa mwalimu kutumia mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji wa somo hili zitakazokuza stadi za karne ya 21 zikiwemo ubunifu, mawasiliano, ushirikiano, fikra tunduizi na utatuzi wa changamoto.

2.0 Malengo Makuu ya Elimu

Malengo makuu ya elimu Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

- (a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujamini;
- (b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;
- (c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;
- (d) Kuelewa na kulinda tunu za taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya taifa;

- (e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;
- (f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;
- (g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na
- (h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

3.0 Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI

Malengo ya Elimu ya Sekondari kidato cha V-VI ni:

- (a) Kuimarisha, kupanua na kuendeleza uelewa wa kina wa maarifa, stadi, na mwelekeo alioupata katika elimu ya sekondari kidato I-IV;
- (b) Kulinda mila na desturi, tunu za taifa, demokrasia, kuthamini haki za binadamu na za kiraia, na wajibu na majukumu yanayoendana na haki hizo;
- (c) Kukuza tabia ya kujiamini na uwezo wa kujifunza kwenye nyanja mbalimbali zikiwemo sayansi na teknolojia, maarifa ya kinadharia na kiufundi;
- (d) Kuimarisha matumizi ya lugha katika mawasiliano ya kitaaluma;
- (e) Kuimarisha uwajibikaji katika masuala mtambuka ya kijamii yakiwemo afya, usalama, usawa wa kijinsia, na utunzaji endelevu wa mazingira;
- (f) Kujenga ujuzi na stadi mbalimbali zitakazomwezesha kujajiri, kuajiriwa, na kuyamudu maisha kwa kutumia vizuri mazingira yake; na
- (g) Kumwandaa mwanafunzi kuijunga na vyuo vya elimu ya kati na elimu ya juu.

4.0 Umahiri wa jumla Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI

Umahiri ni uwezo wa kutenda jambo kwa usahihi na ufanisi uliokusudiwa. Umahiri hujengwa na mwanafunzi kwa kutenda shughuli mbalimbali kwa ufanisi. Umahiri wa jumla wa Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI ni:

- (a) Kutumia maarifa na stadi alizozipata katika ngazi ya elimu ya sekondari hatua ya chini kuimarisha na kupanua uelewa wake kitaaluma;
- (b) Kuthamini uraia, tunu za taifa, na haki za binadamu na za kiraia;
- (c) Kujiamini katika ujifunzaji wa nyanja mbalimbali zikiwemo sayansi na teknolojia, maarifa ya kinadharia na kiufundi;
- (d) Kutumia stadi za lugha katika mawasiliano ya kitaaluma;
- (e) Kutumia maarifa ya masuala mtambuka kumudu mazingira yanayomzunguka;
- (f) Kutumia ujuzi na stadi alizozipata kumwezesha kujajiri, kuajiriwa na kuyamudu maisha kwa kutumia vizuri mazingira yake; na
- (g) Kuonesha utayari wa kujeungu na ngazi ya elimu inayofuata.

5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi

Muhtasari wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI una umahiri mkuu na umahiri mahususi kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na.1.

Jedwali Na. 1: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi
1. Kulinda historia ya Tanzania, urithi na maadili ya taifa	1.1. Kumudu historia, utambulisho na maadili ya taifa 1.2. Kutathmini mchango wa historia na urithi katika kuchangia maendeleo ya taifa 1.3. Kutumia fursa mbalimbali zitokanazo na historia na urithi wa Tanzania kujenga ushirikiano na kukuza biashara ya kimataifa
2. Kumudu historia ya Tanzania na maadili kabla ya ukoloni	2.1. Kutathmini vichocheo vya maendeleo ya jamii za Kitanzania na maadili yake kabla ya ukoloni 2.2. Kuelezea uhusiano wa jamii za Kitanzania na jamii nyingine duniani kabla ya ukoloni 2.3. Kuhusianisha mapokeo ya mifumo ya kihistoria katika kuelezea maadili ya Kitanzania
3. Kumudu historia ya Tanzania na maadili wakati wa ukoloni, 1890-1960	3.1. Kutathmini ukoloni kama nguvu laini (<i>soft power</i>) ya kujenga mwelekeo mpya wa jamii 3.2. Kuchambua mchango wa ukoloni katika mfumo wa maadili ya Kitanzania
4. Kumudu historia ya ujenzi wa taifa la Tanzania na maadili katika kipindi cha 1961- 1966	4.1. Kumudu chimbuko la ukoloni mamboleo 4.2. Kutathmini mabadiliko ya mifumo ya ulinzi na usalama wa taifa 4.3. Kuchambua visababishi vya mabadiliko ya Sera ya mambo ya nje na uhusiano ya kimataifa 4.4. Kutathmini mchango wa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar katika kudumisha uhuru, umoja na amani ya kitaifa
5. Kutathmini ujenzi wa taifa na maadili yake wakati wa Azimio la Arusha, 1967-1985	5.1. Kuchambua chimbuko la Azimio la Arusha na matokeo yake kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kimaadili 5.2. Kutathmini nafasi ya Tanzania katika kujenga uhusiano wa kikanda

6. Kutathmini historia ya Tanzania na maadili wakati wa uliberali, 1986 hadi sasa	6.1. Kutafsiri mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kimaadili katika kipindi cha uliberali na utandawazi kuanzia 1986 hadi sasa
7. Kufanya kazi mradi ya historia ya Tanzania na maadili	7.1 Kufanya kazi mradi ya historia ya Tanzania na maadili

6.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi katika Mchakato wa Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji unategemea ushirikiano madhubuti baina ya mwalimu, mwanafunzi na mzazi/mlezi katika kutekeleza majukumu mbalimbali. Majukumu hayo ni kama yafuatayo:

6.1 Mwalimu

Mwalimu anatarajiwaa:

- (a) Kumwezesha mwanafunzi kujifunza na kupata umahiri uliokusudiwa katika somo la Historia ya Tanzania na Maadili;
- (b) Kutumia mbinu za ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia umri, mahitaji anuai na uwezo wa mwanafunzi ili kumwezesha:
 - (i) Kujenga umahiri unohitajika katika Karne ya 21;
 - (ii) Kushiriki ipasavyo katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji;
- (c) Kutumia mbinu shirikishi zinazomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji zikiwemo zile zitakazomwezesha kufikiri, kutafakari na kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali;
- (d) Kuandaa darasa salama lenye mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia;

- (e) Kutengeneza na kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia;
- (f) Kufanya upimaji endelevu mara kwa mara kwa kutumia zana na mbinu za upimaji na tathmini zinazopima nadharia na vitendo zikiwemo bunguabongo, orodhahakiki, majoribio, dodoso, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo (kazi binafsi, kazi za vikundi), kazimradi na mkoba wa kazi. Zana na mbinu nyingine ni majoribio kwa vitendo, uwasilishaji, mitihani ya muhula na mtihani wa mwisho;
- (g) Kuhakikisha kuwa ujifunzaji na ufundishaji linafanyika kwa haki na usawa kwa kila mwanafunzi bila kujali tofauti zao;
- (h) Kumlinda mwanafunzi awapo shulenii;
- (i) Kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi ya kila siku;
- (j) Kubaini mahitaji ya mwanafunzi na kutoa afua stahiki;
- (k) Kushirikisha wazazi/walezi na jamii katika hatua mbalimbali za ujifunzaji wa mwanafunzi; na
- (l) Kuchopeka masuala mtambuka na TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.

6.2 Mwanafunzi

- (a) Kuwa mtendaji mkuu katika mchakato wote wa ujifunzaji;
- (b) Kushiriki katika shughuli mbalimbali za ujifunzaji ndani na nje ya darasa ili kupata umahiri uliokusudiwa; na
- (c) Kushiriki katika kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo vitabu vya kiada, ziada na machapisho mengine kutoka katika maktabamtandao.

6.3 Mzazi

Mzazi/ Mlezi anatarajiwa:

- (a) Kusimamia na kufuutilia maendeleo ya mtoto katika ujifunzaji;
- (b) Pale inapowezekana kumsimamia mtoto kutekeleza kazi zake za kitaaluma;
- (c) Kuhakikisha kuwa mazingira ya nyumbani ni rafiki na salama yanayowezesha ujifunzaji;
- (d) Kufuutilia mwenendo wa tabia ya mtoto;
- (e) Kumpatia mtoto vifaa vyote vinavyohitajika katika shughuli ya ujifunzaji;
- (f) Kuhakikisha mwanafunzi anapata mahitaji muhimu; na
- (g) Kumfundisha mtoto juu ya umuhimu na thamani ya elimu pamoja na kumhimiza kujifunza kwa bidii.

7.0 Mbinu Pendekewza za Ufundishaji na Ujifunzaji

Mbinu za Ufundishaji na ujifunzaji ni msingi katika kujenga umahiri kwa mwanafunzi. Muhtasari huu unapendekeza mbinu za ufundishaji na ujifunzaji kwa kila shughuli. Miongoni mwa mbinu hizo ni ziara za kimasomo, kazimradi na kazi za vitendo. Hata hivyo mwalimu anashauriwa kutumia mbinu nyingine kama hizo kulingana na muktadha wa ujifunzaji.

8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji

Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unahitaji zana mbalimbali. Hivyo, mwalimu na mwanafunzi wanapaswa kushirikiana katika kuandaa au kufaragua zana zinazopatikana katika mazingira ya shulenii na nyumbani pindi vinapohitajika. Mwalimu na mwanafunzi wanapaswa kutafuta taarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali ili kuwezesha kikamilifu mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Orodha ya vifaa vilivyothibitishwa kwa ajili ya rejea vitatolewa na TET.

9.0 Upimaji

Upimaji wa maendeleo ya ujifunzaji ni suala muhimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Historia ya Tanzania na maadili. Mwalimu anashauriwa kuwa na uwanja mpana wa uchaguzi wa mbinu na zana za upimaji wa Somo la Historia ya Tanzania na Maadili. Upimaji utafanyika sambamba na masomo mengine yanayofundishwa katika ngazi ya Sekondari Kidato cha V-VI. Upimaji wa maendeleo utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji. Kwa hiyo, zana/vifaa vinavyotumika katika upimaji ni pamoja na mazoezi, maswali ya ana kwa ana, majaribio, hojaji, mkoba wa kazi, kazimradi, na mitihani. Upimaji utahusisha 70% ya mtihani wa mwisho utakaotolewa kidato cha VI na Baraza la Mitihani la Taifa pamoja na upimaji endelevu (30%), kama inavyooneshwa kwenye jedwali Na.2.

Jedwali Na. 2: Mgawanyo wa Alama za Upimaji

Aina ya Upimaji	Kidato cha V	Kidato cha VI
Mtihani wa muhula wa kwanza	05%	06%
Mtihani wa muhula wa pili	05%	-
Kazimradi	-	07%
Mtihani wa Utimilifu	-	07%
Mtihani wa Taifa	-	70%
JUMLA		100%

10 .0 Idadi ya Vipindi

Muhtasari wa Somo Historia ya Tanzania na Maadili Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutendwa na mwanafunzi. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 40. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni vinne (4) kwa wiki kwa kidato cha V - VI.

11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Muhtasari wa Somo la Historia ya Tanzania na Maadili Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI umebeba maudhui ambayo yamepangiliwa katika vipengele saba ambavyo ni umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za kutendwa na mwanafunzi, mbinu zinazopendekezwa, vigezo vya upimaji, vifaa/zana, na idadi ya vipindi. Maudhui hayo yameoneshwa katika majedwali Na. 2 na 3.

Kidato cha V

Jedwali Na. 3: Maudhui ya Kidato cha V

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
1. Kulinda historia ya Tanzania, urithi na maadili ya taifa	1.1 Kumudu historia, utambulisho na maadili ya taifa	(a)Kueleza dhana na uhusiano wa kinadharia uliopo kati ya historia, utambulisho na maadili ya taifa	BunguaBongo ongoza wanafunzi kueleza dhana na uhusiano wa kinadharia uliopo kati ya historia, utambulisho na maadili Kisamafunzo wape wanafunzi kisa kuhusu maana, umuhimu na uhusiano wa kinadharia uliopo kati ya msamati hiyo ili kujenga uelewa Maswali na majibu toa maswali mbalimbali kuhusu dhana na uhusiano wa kinadharia uliopo kati ya historia, utambulisho na maadili ya taifa	Dhana na uhusiano wa kinadharia uliopo kati ya historia, utambulisho na maadili ya taifa vimeelezwa kwa usahihi	Matini, ramani ya Tanzania, bendera ya Tanzania, na chati yenye kuonesha uhusiano kati ya historia, utambulisho na maadili ya taifa	24

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji	Vigezo vyta upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
		(b) Kujadili misingi ya kihistoria iliyounda utambulisho na maadili ya taifa	<i>Majadiliano ya vikundi</i> wagawe wanafunzi katika makundi na waongoze kujadili misingi ya kihistoria iliyounda utambulisho na maadili ya taifa na mwisho kila kundi wafanye wasilisho darasani ili kupata ulewa wa pamoja	Misingi ya kihistoria iliyounda utambulisho na maadili ya taifa imejadiliwa kwa kina		
		(c) Kuchambua nafasi ya historia na maadili katika kujenga fahari ya taifa	<i>Bunguabongo</i> ongoza wanafunzi kuelezea nafasi ya historia na maadili katika kujenga fahari ya jamii yake <i>Kisa fikirika (scenario)</i> tengeneza kisa na	Nafasi ya historia na maadili katika kujenga fahari ya taifa imechambuliwa kwa usahihi	Matini, bendera ya Tanzania, michoro, picha ya urithi wa taifa	

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
			maswali kuhusu nafasi ya historia na maadili katika kujenga fahari ya taifa ili kuibua majadiliano ya kisa hicho na uhalisia wake			
		(d) Kutathmini nafasi ya Tunu za taifa na maadili katika kujenga misingi ya uongozi bora	<p><i>Fikiri-andika-jozisha shirikisha</i> ongoza wanafunzi kushiriki kufikiri kuhusu nafasi ya tunu na maadili kujenga misingi ya uongozi.</p> <p><i>Tafakuri</i> ongoza wanafunzi kufanya tafakuri kuhusu nafasi ya tunu za taifa na maadili katika kujenga misingi ya uongozi bora</p>	Nafasi ya tunu za taifa na maadili katika kujenga misingi imara ya uongozi imetathminiwa kikamilifu	Chati yenye kuonesha tunu za taifa, hotuba za viongozi wa kitaifa	

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji	Vigezo vyatupimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
		(e) Kubaini mikakati ya kulinda historia, utambulisho na maadili ya taifa	<p><i>Changanyakete</i> wagawanye wanafunzi katika makundi kisha waelekeze kubainisha mikakati ya kulinda historia, utambulisho na maadili katika jamii zao</p> <p><i>Kisamafunzo</i> wape wanafunzi kisa na waelekeze kubaini mikakati ya kulinda historia, utambulisho na maadili ya taifa. Uliza maswali chokonozi ili kuibua fikra tunduizi kuhusu kisamafunzo.</p>	Mikakati ya kulinda historia, utambulisho na maadili ya taifa imebainishwa kwa usahihi		

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
	1.2 Kutathmini mchango wa historia na urithi katika kuchangia maendeleo ya taifa	(a)Kufafanua dhana ya urithi wa taifa (b)Kubaini historia na urithi wa taifa katika maeneo mbalimbali nchini	Bunguabongo waongoze wanafunzi katika makundi kujadili kuhusu maana na sifa za urithi wa taifa Majadiliano waongoze wanafunzi katika makundi kushiriki mjadala juu ya maana na sifa za urithi wa Taifa Kisamafunzo wape wanafunzi kisa kuhusu historia na urithi wa taifa ili waweze kupata picha halisi Utafiti mdogo waongoze wanafunzi kufanya utafiti kubainisha historia na urithi wa taifa katika maeneo yanayowazunguka	Dhana ya urithi wa taifa imefafanuliwa kwa usahihi Historia na urithi wa taifa katika maeneo mbalimbali nchini imebainishwa kwa usahihi	Matini, chati/ michoro/picha yenye kuonesha urithi wa taifa Matini, chati/ michoro/picha yenye kuonesha urithi wa taifa	24

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
		<p>(c) Kujadili mchango wa historia na urithi katika maendeleo ya taifa</p> <p>(d) Kuchambua uhusiano uliopo kati ya maadili na urithi katika kuleta maendeleo ya taifa</p>	<p>Bunguabongo ongoza wanafunzi kujadili juu ya mchango wa historia na urithi kwa maendeleo katika maeneo yao</p> <p>Majadiliano ongoza wanafunzi katika vikundi kujadili mchango wa historia na urithi katika maendeleo ya taifa</p> <p>Changanyakete ongoza wanafunzi katika kujadili uhusiano uliopo kati ya maadili na urithi katika kuleta maendelo kwenye maeneo yao.</p> <p>Majadiliano ongoza wanafunzi kudadavua kwa kina uhusiano uliopo kati ya maadili na urithi katika kuleta maendeleo ya taifa</p>	<p>Mchango wa historia na urithi katika maendeleo ya taifa umejadiliwa kwa kina</p> <p>Uhusiano uliopo kati ya maadili na urithi katika kuleta maendelo ya taifa umechambuliwa kwa kina</p>	<p>Matini, chati/ michoro/picha yenyе kuonesha urithi wa taifa, maswali elekezi</p> <p>Matini, chati yenyе kuonesha uhusiano kati ya maadili, urithi na maendeleo ya taifa, kisamafunzo</p>	

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji	Vigezo vyta upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
		(e) Kujadili njia bora za uhifadhi wa urithi ili kuleta maendeleo endelevu kwa taifa	Bunguabongo ongoza wanafunzi kujadili kuhusu njia anuwai za uhifadhi wa urithi wanaoujua katika maeneo yao Majadiliano ongoza wanafunzi kujadiliana kwa kina njia bora za uhifadhi wa urithi ili kuleta maendeleo endelevu kwa taifa	Njia bora za uhifadhi wa urithi ili kuleta maendeleo endelevu kwa taifa zimejadiliwa kwa kina	Matini, maswali elekezi, chati ya kuonesha njia za uhifadhi wa urithi	

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji	Vigezo vyatupimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
1.3 Kutumia fursa mbalimbali zitokanazo na historia na urithi wa Tanzania kujenga ushirikiano na kukuza biashara ya kimataifa	(a)Kubaini fursa za kiuwekezaji zitokanazo na vivutio vyatupimaji na urithi wa Tanzania	Mtaalamu mualikwa elekeza mtaalamu kuelezea kuhusu fursa za kiuwekezaji zitokanazo na vivutio vyatupimaji na urithi wa Tanzania <i>Maswali na majibu</i> toa maswali kwa wanafunzi kuhusu fursa za kiuwekezaji zitokanazo na vivutio vyatupimaji na urithi wa Tanzania	Fursa za kiuwekezaji zitokanazo na vivutio vyatupimaji na urithi wa Tanzania zimebainishwa kikamilifu	Ramani/picha za urithi na vivutio vyatupimaji na urithi na vivutio vyatupimaji na urithi wa Tanzania zimebainishwa kikamilifu	13	

Umahiri mkuu	Umahiri mahuusi	Shughuli za ujifunzaji	Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
		(b)Kujadili nafasi ya historia na urithi wa Tanzania katika kujenga ushirikiano na kukuza biashara ya kimataifa	<i>Kisafikirika (scenario)</i> ongoza wanafunzi katika makundi madogo madogo na wape scenario inayoonesha umuhimu wa historia na urithi katika kujenga ushirikiano na biashara ya kimataifa <i>Majadiliano</i> ongoza wanafunzi kujadili nafasi ya historia na urithi wa Tanzania katika kujenga ushirikiano na kukuza biashara ya kimataifa	Nafasi ya historia na urithi wa Tanzania katika kujenga ushirikiano na kukuza biashara ya kimataifa imejadiliwa kwa kina	Maswali elekezi, matini, Makala kwenye magazeti	

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji	Vigezo vyatupimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
		(c) Kubaini vitendo vyakimaadili na visivyo vyakimaadili vinavyoweza kukuza au kudumaza fursa zitokanazo na historia na urithi	Bunguabongo ongoza wanafunzi kujadiliana kuhusu vitendo vyamaadili na visivyo vyamaadili vinayokuza au kudumaza fursa katika maeneo ya karibu Changanyakete ongoza wanafunzi katika makundi madogo madogo, elekeza wabainishe vitendo vyakimaadili vinavyokuza na wengine visivyo vyakimaadili vinavyodumaza fursa za kihistoria na urithi	Vitendo vyakimaadili na visivyo vyakimaadili vinavyoweza kukuza au kudumaza fursa zitokanazo na historia na urithi vimebainishwa kikamilifu	Chati yenye kuonesha matendo ya kimaadili na yasiyo ya kimaadili, picha, visamafunzo kuhusu uharibifu wa historia na urithi, matini	

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji	Vigezo vyta upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
2. Kumudu historia ya Tanzania na maadili kabla ya ukoloni	2.1 Kutathmini vichocheo vya maendeleo ya jamii za Kitanzania na maadili yake kabla ya ukoloni	(a) Kueleza vichocheo vya maendeleo ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni	Bunguabongo ongoza wanafunzi kujadili vichocheo vya maendeleo katika jamii zao Fikiri-andika-jozisha- shirikisha ongoza wanafunzi kushiriki kuhusu vichocheo vya maendeleo ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni	Vichocheo vya maendeleo ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni vimeelezwa kwa usahihi	Matini, vitu hali (zana za kale)	14

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji	Vigezo vyta upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
		(b) Kutathmini maadili ya jamii za Kitanzania na namna yalivyochochea maendeleo kabla ya ukoloni	<i>Maswali na majibu</i> ongoza wanafunzi kutoa ufafanuzi kuhusu maadili ya jamii na umuhimu wake kwenye maendeleo ya jamii zao <i>Tafakuri (self-reflection)</i> ongoza wanafunzi kutafakari namna maadili ya jamii za Kitanzania yalivyochochea maendeleo kabla ya ukoloni	Maadili ya jamii za Kitanzania na namna yalivyochochea maendeleo kabla ya ukoloni yametathminiwa kwa kina	Chati yenye kuonesha uhusiano wa maadili na maendeleo ya jamii, matini	

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
		(c) Kuchambua mifumo ya kusimamia maadili katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni	Kisamafunzo andaa na ongoza wanafunzi kutafari kisamafunzo kuhusu mifumo inayosimamia maadili katika jamii mbalimbali Fikiri-andika-jozisha-shirikisha ongoza wanafunzi na kuchunguza jinsi mifumo ya kusimamia maadili katika jamii za Kitanzania ilivyokuwa kabla ya ukoloni	Mifumo ya kusimamia maadili katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni imechambuliwa kwa kina	Matini, chati ya mifumo ya maadili	

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji	Vigezo vyatupimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
	2.2. Kuelezea uhusiano wa jamii za Kitanzania na jamii nyingine duniani kabla ya ukoloni	(a) Kuchambua uhusiano wa jamii za Kitanzania na jamii nyingine za Kiafrika kabla ya ukoloni	Ramani andaa na waoneshe ramani ikiwa na alama za uhusiano baina ya jamii husika waichunguze na waongoze kuchambua uhusiano huo. Tafakuri (Self-reflection) ongoza wanafunzi kutafakari na kuchambua uhusiano wa jamii za Kitanzania na jamii nyingine za Kiafrika kabla ya ukoloni	Uhusiano wa jamii za kitanzania na jamii nyingine za kiafrika kabla ya ukoloni umechambuliwa kwa kina	Picha/michoro ya jamii za kabla ya ukoloni na ramani	17

Umahiri mkuu	Umahiri mahuusi	Shughuli za ujifunzaji	Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
		(b) Kuchambua uhusiano baina ya jamii za Kitanzania na zile za Ulaya, Mashariki ya Kati na Mashariki ya Mbali	Ramani andaa na waoneshe ramani ikiwa na alama za uhusiano baina ya jamii husika waichunguze na waongoze kuchambua uhusiano huo. Majadiliano Ongoza wanafunzi kuchambua uhusiano wa jamii za Kitanzania na hizo za nje (zile za Ulaya, Mashariki ya Kati na Mashariki ya Mbali)	Uhusiano baina ya jamii za Kitanzania na zile za Ulaya, Mashariki ya Kati na Mashariki ya Mbali umechambuliwa kwa kina	Chati ya uhusiano, matini, ramani/ picha/michoro	

Umahiri mkuu	Umahiri mahuusi	Shughuli za ujifunzaji	Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji	Vigezo vyta upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
		(c) Kuhusianisha mifumo ya maadili ya jamii nyingine duniani na jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni	<i>Kisamafunzo</i> andaa na ongoza wanafunzi kusoma kisa chenye mada ya mifumo ya maadili ya jamii mbalimbali duniani <i>Tafakuri</i> ongoza wanafunzi kutafakari uhusiano wa mifumo ya maadili ya jamii nyingine duniani na jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni	Mifumo ya maadili ya jamii nyingine duniani na jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni imehusianishwa kwa usahihi	Chati ya mifumo ya maadili, matini	

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Mbinu zinazopendekezwa za ufundishaji na ujifunzaji	Vigezo vyatupimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
